

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA NANE

KIKAO CHA NANE

06 FEBRUARI, 2020



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA NANE

KIKAO CHA NANE – TAREHE 06 FEBRUARI, 2020

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2019.



MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2019.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

96. MHESHIMIWA JULIUS KALANGA LAIZER (MONDULI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mji wa Mto wa Mbu ni Mji wa kitalii na unaingiza mapato mengi ya kitalii lakini unakabiliwa na tatizo la miundombinu ya barabara:-

- (a) Je, nini mkakati wa Serikali kuupatia Mji wa Mto wa Mbu angalau km 5 za lami;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa barabara ya Mto wa Mbu mpaka Loliondo kwa kiwango cha lami ili kusaidia mradi wa kimkakati wa magadi Engaruka;
- (c) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya Mhe. Rais ya kuweka lami barabara ya Ngarash mpaka Monduli juu kwa Sokoine.

97. MHESHIMIWA QAMBALO WILLY QULWI (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mabaraza ya Ardhi ya

Kata ni vyombo muhimu sana katika kutatua migogoro ya Ardhi; hata hivyo changamoto kubwa ni uwezeshaji (chakula na nauli) kwa Wajumbe wa Mabaraza hayo ili wafanye kazi zao kwa weledi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Wajumbe wa Mabaraza hayo wanawezeshwa ili waweze kutoa haki.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

98. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Kumekuwa na ongezeko kubwa la Watoto wa Mitaani Jijini Dar es Salaam hali ambayo inakosesha Watoto hao haki zao za msingi kama elimu na malezi bora:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kukabiliana na tatizo hilo.

WIZARA YA KILIMO:

99. MHESHIMIWA MARTIN MTONDA MSUHA (MBINGA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha Sheria ya Vyama vya Ushirika ili kuondoa mapungufu yaliyopo, hususan kwenye upande wa Uanachama na kuipa Serikali nguvu za Kisheria juu ya Vyama vya Ushirika.

100. MHESHIMIWA AZZA HILALY HAMAD (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itachimba Bwawa kwa ajili ya kuboresha mradi wa umwagiliaji katika Kijiji cha Nyida.

WIZARA YA NISHATI:

101. MHESHIMIWA MARY PIUS CHATANDA (KOROGWE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Umeme umekuwa ukikatika mara kwa mara Korogwe na kusababisha uharibifu wa mali za Wananchi:-

Je, ni lini tatizo hilo litapatiwa ufumbuzi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

102. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Ni kosa la jinai kwa mtu au

vyombo vya habari kutoa, kuandika, kusambaza au kutangaza habari za uongo:-

Je, Jeshi la Polisi linachukua hatua gani stahiki kwa Watu au vyombo vya habari vinavyofanya makosa hayo.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

103. MHESHIMIWA ISSA ALI MANGUNGU (MBAGALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Eneo la kipande cha barabara ya Kilwa – Rangi Tatu – Kongowe limeharibika vibaya na kusababisha foleni na ajali nyingi:-

- (a) Je, ni lini Serikali itajenga barabara hiyo kikamilifu kwa kiwango cha lami ili kuondoa kero hizo;
- (b) Je, ahadi ya Mhe. Rais ya kujenga kipande hicho kwa njia nne mpaka Kongowe itanza lini;
- (c) Daraja la Mto Mzinga katika kipande hicho lipo katika hali mbaya na hatarishi; Je, ni lini Serikali itajenga daraja jipya kama alivyoahidi Mhe. Rais wakati akiwa Waziri wa Ujenzi.

**104. MHESHIMIWA OLIVER DANIEL
SEMUGURUKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kivuko kilichopo Bukoba Vijijini Kyanyabasa hakikidhi viwango kabisa:-

Je, ni lini Serikali itaweka kivuko au daraja litakalokidhi viwango.

V. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2019.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2019.

**DODOMA
06 FEBRUARI, 2020**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**